# Matokeo ya Usawa
# 2013 -2017

COMMS-0413-126

## Jinsi tulivyounda matokeo yetu ya usawa

Tuliangalia taarifa yote tunazoweka na kutumia kuhusu usawa. Tulizingatia ni kwa jinsi gani vizuri sisi hutimiza majukumu yetu ya usawa na nini zaidi tunaweza kufanya. Tumechapisha habari hii katika ripoti yetu Kuelekea Usawa (2013) ambayo inaonyesha hatua za kuendeleza wajibu wa usawa wa sekta ya umma kwa miaka miwili ijayo.

Kuelewa vizuri mahitaji ya watu na matarajio yetu tulisikiliza ujumbe kutoka kwa makundi ya usawa yanayowakilisha umri, ulemavu, uwekaji upya wa jinsia, ndoa na ushirikiano wa umma, mimba na uzazi, asili, dini au imani, jinsia na mwelekeo wa kijinsia.

Tutatumia hatua zilizoonyeshwa katika ripoti yetu Kuelekea Usawa (2013) kupima maendeleo kuelekea matokeo yetu ya usawa na kwa hiyo ripoti hii lazima ionekana kama kufuatilia taarifa iliyotathminiwa katika ripoti hiyo.

Usawa na Uongozi wa Tume ya Haki za Binadamu inahimiza kauli juu ya matokeo kutamaniwa na kuhusishwa na malengo ya shirika na matokeo.

Kila matokeo ambayo tumeanzisha yanahusishwa na angalau mpango moja wetu wa matokeo ya shirika.

- Matokeo ya 1: Ubora wa huduma nchini Uskoti inaendelea kuwa nzuri.
- Matokeo ya 2: Watu kuelewa ubora wa huduma wanapaswa kutarajia na kuwa na uzoefu mzuri wa huduma zilizoko kwa mahitaji yao, haki, na hatari.
- Matukio ya 3: Ukaguzi wa Matunzo hutenda vizuri na kwa ufanisi kama shirika huru la uchunguzi na kufanya kazi vizuri kwa kushirikiana na mashirika mengine.

Kushauriana juu ya maoni ya watuwenye sifa zilizolindwa ilifanywa kupitia utafiti wa mtandao na kuwasiliana moja kwa moja na aina mbalimbali ya makundi ya usawa na mashirika nchini Uskoti. Tulihakikisha kwamba makundi haya na mashirika yalikuwa ni wawakilishi wa kila sifa tisa zilizolindwa.

Wafanyikazi wa Ukaguzi wa Matunzo kutoka kote katika maeneo yetu ya kazi, na kutoka kote nchini Uskoti, wamehusika katika kutambua ushahidi na upungufu katika usawa wa kazi zetu.

Tumejihusisha na Baraza la Uskoti la Huduma za Jamii na Uboreshaji Huduma za Afya nchini Uskoti kuendeleza kauli ambazo zinaeleweka kwa watu ambao wanazisoma na ambayo inaweza kufanya tofauti kubwa kwa maisha ya watu walioathirika na ukosefu wa usawa na ubaguzi.

Katika utekelezaji wa kazi hii sisi tumekuwa na mawasiliano ya moja kwa moja na Ukaguzi wa Uskoti, Elimu ya Uskoti, Uboreshaji Afya nchini Uskoti, Mkuu wa Ukaguzi wa Jeshi la Polisi ya Uskoti na Baraza la Uskoti la Huduma za Jamii.

## Matokeo ya Usawa

1. **Tunachukua hatua madhubuti ya kulinda na kukuza haki za watu wa umri wote, ikiwa ni pamoja na mageuzi ya jinsia, mwelekeo wa kijinsia, wale wenye ulemavu, wa asili zote na watu wa imani yoyote au wasiokuwa wa imani.**

   Matokeo ya 2 ya Mpango wa Shirika

2. **Watu wa umri wote na jinsia ikiwa ni pamoja na mageuzi ya jinsia, mwelekeo wa kijinsia, wale wenye ulemavu, wa asili zote na watu wa imani yoyote au wasiokuwa na imani, kupokea matunzo mema na huduma za kazi za kijamii.**

   Matokeo ya 1 ya Mpango wa Shirika
   Matokeo ya 2 ya Mpango wa Shirika
   Matokeo ya 3 ya Mpango wa Shirika

3. **Watu zaidi wa umri wote na jinsia zote ikiwa ni pamoja na mageuzi ya jinsia, mwelekeo wa kijinsia, wale wenye ulemavu, wa asili zote na watu wa imani yoyote au wasiokuwa nayo wanatuambia kuhusu matunzo na huduma za kazi za kijamii wanazopitia na kutaka.**

   Matokeo ya 1 ya Mpango wa Shirika

4. **Wafanyakazi wetu, katika madaraja yote na kazi, huonyeza vizuri na kusaidia mahitaji ya watu tunaowahudumia.**

   Matokeo ya 1 ya Mpango wa Shirika
   Matokeo ya 2 ya Mpango wa Shirika
   Matokeo ya 3 ya Mpango wa Shirika

## Kuelekea matokeo ya usawa: Mpango wa kutenda.

| Wajibu mkuu | Matokeo ya Usawa | Kukosekana kwa usawa | Hatua |
|---|---|---|---|
| Kuondoa ubaguzi, unyanyasaji na uonevu | Tunachukua hatua madhubuti ya kulinda na kukuza haki za watu wa umri wote na jinsia ikiwa ni pamoja na mageuzi ya jinsia, mwelekeo wa kijinsia, wale wenye ulemavu, wa asili zote na watu wowote au wasiokuwa na imani au imani. | Makundi ikiwa ni pamoja na Scottish Transgender Alliance na Lesbian Gay Bisexual Transgender Youth Scotland, wameonyesha madhara ya uonevu, ubaguzi na unyanyasaji katika maisha ya watu, ikiwa ni pamoja na wale wa vijana. Kusababisha kuhamisha makazi, ukosefu wa makazi, matumizi mabaya katika mahusiano ya ndani, unyanyasaji kutoka kwa wageni, uvamizi wa kimwili na wa kijinsia.<br><br>Makundi haya pia yanakampenia haki sawa katika ndoa na ushirikiano wa raia na kuondoa ubaguzi na unyanyasaji katika elimu, mafunzo na kazi. | Tutakusanya, kutathmini na kutumia usawa taarifa zinazohusiana na usajili, ukaguzi, malalamiko, utekelezaji na matukio makubwa katika mwaka 2013/15.<br><br>Tutafuatilia jinsi miongozo ya utendaji wetu inazingatia Usawa na utofauti wanafanya katika kushughulikia tofauti za usawa. 2013/15.<br><br>Tutachapisha habari kuhusu kiwango ambacho wenzi wa mipango ya jumuia wanakabiliana kwa mafanikio na kufunga mapengo ya matokeo kwa njia ya ufanisi wa kuzuia na kuingilia kati mapema.<br><br>Tutazingatia matokeo yanayoonekana katika kuboresha nafasi za maisha ya watoto wapweke na vijana.<br><br>Tutafuatilia rekodi ya matukio ya wafanyakazi ya watu wenye tabia zilizolindwa na kutumia taarifa hii kupunguza ubaguzi, uonevu, unyanyasaji au mwenendo mwingine wowote uliopigwa marufuku na Sheria ya Usawa ya 2010 dhidi ya wafanyakazi wetu.<br><br>Tutaongeza uelewa wa taarifa yetu wya histleblowing miongoni mwa wafanyakazi wetu ili ubaguzi, uonevu, unyanyasaji unaopitiwa katika maeneo ya kazi yaweze haraka kusemwa na kushughulikiwa.2013-15<br><br>Kuendeleza wajibu wa usawa tunapanga kukusanya, kutathmini na kutumia taarifa ya usawa kuhusu malalamiko na matukio ya kinidhamu na ufichuzi katika mwaka 2013/15. |

| Wajibu mkuu | Matokeo ya Usawa | Kukosekana kwa usawa | Hatua |
|---|---|---|---|
| Usawa Mahiri wa Fursa | Watu wa umri wote na jinsia ikiwa ni pamoja na mageuzi ya jinsia, wale wenye ulemavu au ambao wametoka kwa makundi madogo ya jamii na watu wowote au wasiokuwa na imani, wanapata huduma ya matu nzo mazuri na kuboresha huduma za kijamii. | Ushirikishwaji Uskoti inaonyesha uhusiano kati ya ulemavu na matatizo ya kujifunza na kupunguzwa kusoma na kuandika, viwango vya mapato, ajira, kunyimwa na matumizi ya tovuti.<br><br>Kufikia huduma na huduma za mtandaoni ni tatizo la kawaida linalokabiliwa na watu wenye ulemavu ambao wanakabiliwa na kukosekana kwa usawa kwa sababu wao wanatarajiwa kutumia mifumo iliyoundwa kukidhi mahitaji yao, au ambayo hawana.<br><br>Funga Pengo ni kikundi cha usawa wa kijinsia ambao wanafanya kazi ya kushughulikia pengo la mshahara wa kikundi. Wanaonyesha kwamba hii inachangia viwango vya juu vya umaskini kwa wanawake na watoto na umaskini wa mpokeaji pensheni kwa wanawake. | Tutaboresha upatikanaji wa taarifa kwenye tovuti yetu na wavuti zetu ndogo zaidi. Tutachapisha nyaraka zote zilizotafsiriwa kwa ombi la watu binafsi kwenye tovuti yetu. 2013-15<br><br>Tutakagua jinsi ya kufanya utathmini wa athari ya usawa ili kwamba tushauriane na watu zaidi wenye sifa zilizolindwa ambao wanaweza kuathiriwa vibaya na sera ya maendeleo yetu au utekelezaji. 2013-15<br><br>Kuhakikisha sisi tunaendelea kuwaajiri na kukuza wafanyakazi kwa haki. Tutakusanya taarifa zaidi na kufanya uchambuzi wa kina zaidi wa habari ya ajira zetu zinazohusiana na makundi ya sifa zilizolindwa. tutatumia habari hii kuwajulisha wasimamizi wa wafanyikazi mkakati zetu.<br><br>Tutafuatilia utofauti wa kikabila ya wafanyakazi wetu dhidi ya mashirika mengine ili kufikiria ni jinsi gani vizuri sisi tunatekeleza wafanyikazi ambao wanawakilisha maslahi bora ya usawa wa watu wote wanaoishi nchini Uskoti.2013 -15 |

| Wajibu mkuu | Matokeo ya Usawa | Kukosekana kwa usawa | Hatua |
|---|---|---|---|
| Kukuza uhusiano mzuri kati ya wale ambao wanashiriki sifa zilizolindwa na wale ambao hawana | Zaidi ya watu wa umri wote na jinsia ikiwa ni pamoja na mageuzi ya jinsia, mwelekeo wa kijinsia, wale wenye ulemavu au ambao wanatoka kwa makundi ya asili watu wachache na watu wa imani yoyote au wasiokuwa na imani au dhana kutuambia kuhusu matunzo na huduma za kazi ya kijamii wanazopitia na wanazotaka. | Shirika la Kabila la Watu Wachache kila mwaka inasasisha kuhusu ushahidi wa idadi ya mashirika ya watu weusi na mashirika ya kikabila ya watu wachahe na mienendo ya fedha ambayo inaonyesha viwango vya chini sana vya msaada. Utafiti zaidi unaonyesha hasara kubwa kwa wanachama wa jumuiya ya Watu Weusi Walio wachache wanaopata huduma na nafasi za huduma za msaada.<br><br>Kati ya watu 170 Wanaohusishwa ambao wanasaidia kazi yetu, kuna uwakilishi wa chini ya vijana, watu wenye shida ya akili, watu kutoka makundi ya asili ya watu wachache, na watu ambao ni wasagaji, mashoga wanaume wanaofanya mapenzi au wenye kubadilisha jinsia. | Tutaendeleza na kutekeleza mikakati maalum ya kikundi cha mtumiaji - kuweka jinsi ya kuwahusisha vijana zaidi, ni vigumu kufikia makundi ya watu (wale ambao wamepitia kukosa makazi, unyanyasaji wa ndani, matumizi mabaya ya madawa ya kulevya na pombe, huduma za haki ya jinai) na wale wanatoka kwa umuia zenye kabila chache.<br><br>Tutakusanya taarifa ya usawa kutoka kwa watu wote wanaohusika na kutumia hii kuhakikisha kuna uwakilishi kamili wa watu kutoka makundi yote ya sifa zilizolindwa.2013-15<br><br>Sisi kikamilifu tutatafuta kushiriki matokeo ya mazoezi mazuri na vikundi vya usawa. Tutahimiza vikundi vya usawa kuonyesha mifano ya mazoezi mazuri ili tuweze kuzingatia hizi katika maeneo yote ya kazi yetu ya mwaka 2013-15<br><br>Tutashiriki rasilimali zetu na utafiti wa utaalamu katika maendeleo ya mazoea ya ubunifu katika huduma na sekta ya kazi za kijamii.2013-15 |

| Wajibu mkuu | Matokeo ya Usawa | Kukosekana kwa usawa | Hatua |
|---|---|---|---|
| Sehemu zote tatu za wajibu kwa ujumla kama ilivyoelezwa hapo juu. | Wafanyakazi wetu, katika kila daraja na kazi, huonyesha bora na kusaidia mahitaji ya watu wenye sifa zilizolindwa ambao sisi tunawahudumia. | Watu kutoka makundi ya makabila madogo, watu wenye ulemavu, watu ambao ni mashoga, wasagaji, wenye jinsia mbili au mageuzi ya jinsia, wanawake, wazazi wapya na vijana wanaathirika vibaya na viwango vya chini vya mapato, ajira na kunyimwa. | Mpango wa maendeleo ya wafanyakazi wetu ni pamoja na mafunzo ya lazima ya kuhusu usawa na utofauti kwa wafanyakazi wote wapya. Timu ya wafanyakazi wetu ya maendeleo wameunda furushi mafunzo ya wafanyakazi wote na hii itawasilishwa katika mwaka 2013-15<br><br>Tutakagua intranet ya wafanyakazi wetu ili wafanyakazi wamewe kwa urahisi zaidi kutafiti na kurejelea habari muhimu kwa makundi yote ya sifa zilizolindwa. Tutahakikisha kuna viungo vingi zaidi kutoka kwa nyaraka zetu na machapisho kwa vikundi vya usawa ili kusaidia mawasiliano ya moja kwa moja kwa watu ambao hawashiriki sifa zilizolindwa na wale ambao hufanya.2013-15 |

# Kupima Maboresho

Tumeona mpango huu wa utekelezaji kama hati hai ambayo tutarekebisha tukiendelea. Tutapima maendeleo yetu kuelekea kukidhi wajibu wa usawa wa sekta ya umma kama hatua za utekelezaji zilizotambuliwa ndani ya mpango huu zimetimizwa. Kazi zaidi kuhusu mpango wa utekelezaji itafanywa kuhusisha hatua na ubora zilizopo na viashiria muhimu vya utendaji.

Mpango wa utekelezaji na matokeo ya kauli inaweza kurekebishwa kwa msingi wa ushahidi mpya kuhusu masuala ya usawa. Kwa njia hii kazi yetu itakuwa na kuendeshwa na taarifa za sasa za usawa.

# Tarehe ya ukaguzi

Tutaripoti juu ya maendeleo kabla ya tarehe 30 Aprili 2015.

Tutakagua kauli za matokeo kabla ya tarehe 30 Aprili 2017.

**Makao Makuu**
Ukaguzi wa Matunzo
Compass House
11 Riverside Drive
Dundee
DD1 4NY
Simu: 01382 207100
Faksi: 01382 207289

Tuna ofisi kote nchini Uskoti. Kupata ofisi iliyo karibu na wewe, tembelea tovuti yetu au piga simu yetu ya maulizo kwa namba ya Huduma ya Ukaguzi.

**Tovuti: www.careinspectorate.com**
**Barua pepe: enquiries@careinspectorate.com**
**Maulizo ya Ukaguzi wa Matunzo: 0845 600 9527**

Chapisho hili linapatikana katika muundo mwingine na lugha zingine ikiitishwa.

HAPPY TO TRANSLATE

© Matunzo ya Ukaguzi 2013
Imechapishwa na: Communications

Corporate member of Plain English Campaign 420
Committed to clearer communication